

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Anwani ya Simu: "UCHUNGUZI"  
Simu Nambari: 028-2520004  
Nukush028-2520040  
Barua pepe: rbcgeita@pccb.go.tz  
Unapojibu tafadhali taja:



MKUU WA TAKUKURU (M),

S.L. P. 38,  
GEITA,  
TANZANIA.

**JUNI 24, 2020**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.**

**TAKUKURU MKOA WA GEITA YAREJESHA FEDHA ZA MADAI YA WAKULIMA WA  
PAMBA SHILINGI 7,118,200/=**

Kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 30/04/2020 kiliwatuhumu Viongozi wa AMCOS Nne za **NYANZUMLA, NYAKASULWA, KATOMA WAKULIMA NA TUPENDANE** kwa kushindwa kuwalipa wakulima wa pamba wapatao Tisini (90) ambao kwa pamoja wanadai kiasi cha shilingi 8,507,800/= kwa mauzo ya pamba ya msimu wa mwaka 2019/2020.

Kutokana na tuhuma hizo TAKUKURU mkoa wa Geita ilipokea maelekezo kutoka kwa Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Geita ndugu JOPSEPHAT MAGANGA ya kututaka tufanye ufuatiliaji wa fedha za wakulima hao wa Pamba na kuhakikisha zinarejeshwa.

Katika kutekeleza maagizo hayo, TAKUKURU Mkoa wa Geita ilifanya ufuatiliaji na kufanikisha urejeshaji wa kiasi cha shilingi 7,118,200/= kati ya shilingi 8,507,800/= na kiasi cha shilingi 1,389,600/= kilichobaki kinaendelea kurejeshwa kwa awamu.

Tarehe 23/06/2020 Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Geita Bw. Leonidas R. FELIX amekabidhi fedha hizo zilizorejeshwa kiasi cha shilingi 7,118,200/= kwa Katibu Tawala wa Wilaya Geita ndugu THOMAS DIME kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Geita ili fedha hizo ziweze kukabidhiwa kwa wakulima.

Aidha katika makabidhiano hayo Mkuu wa **TAKUKURU** mkoa wa Geita Bwana Leonidas R. FELIX amewaasa Viongozi wa AMCOS mkoani Geita kuwatumikia wakulima kwa uadilifu na kuwataka wajenge tabia ya kuwalipa wakulima fedha zao kwa wakati.

Imetolewa na

**Mkuu wa TAKUKURU (M) GEITA – Bw. Leonidas R. FELIX**